**REGISTRATION INSOLVENCY AND TRUSTEESHIP AGENCY**
WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
**(RITA)**

## RITA ni nini?

RITA ni Wakala wa Serikali katika Wizara ya Katiba na Sheria .Wakala huu umeundwa kutoka iliyokuwa Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu,ambayo hujulikana sana kama vizazi na vifo,Msajili Mkuu wa Ndoa na Talaka au Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu.Maneno haya yote huelezea Ofisi ambayo kwa sasa imebadilishwa na kuwa Wakala kutoka Idara ya Serikali.Kazi zilizokuwa zikifanywa na Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu sasa zinafanywa na RITA vile vile huduma nyingine zitaongezwa ili kukidhi mahitaji ya kijamii.

Mbali na kuandikisha vizazi na vifo RITA inashughulika na:

- Mirathi (wosia)
- Ufilisi
- Upokezi rasmi(Official receiver)
- Muunganisho wa Wadhamini (Incorporation of Trustees)
- Usajili wa watoto wa kuasili. (Adoption)
- Usajili wa ndoa na talaka
- Mdhamini wa serikali (Public Trustee)
- Kutoa ushauri wa kisheria kutokana na shughuli za Wakala
- Kuendesha kesi mahakamani zinazohusiana na shughuli za Wakala.

RITA kama Wakala wa Serikali ina wajibu wa kulinda haki za kimsingi ambapo imeanzisha kitengo cha kuandika na kutunza Wosia.Hii ni kutokana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika jamii baada ya mhusika kufariki,na kutokana na unyanganyi wa mali wakati mmoja wa wanafamilia anapofariki.

Wakala una dhamana ya kusimamia mirathi na uzoefu wetu wa muda mrefu unaonyesha kwamba mtu anapofariki bila ya kuacha wosia kunatokea migogoro, kama vile:

- Familia kunyang'anywa mali.
- Mafarakano baina ya wana familia.
- Kesi za mirathi zinapofunguliwa huchukua muda mrefu kuisha.

### SABABU ZA RITA KUANZISHA KITENGO CHA WOSIA

1. RITA ni chombo cha serikali chenye dhamana ya kusimamia mirathi.
2. Utunzaji wa wosia ni moja ya kazi zilizoainishwa kwenye sheria iliyoanzisha Wakala (Executive Agency Act, Cap 30 1997 .Chini ya Tangazo la Serikali Na. 397 /2005).
3. RITA kama wasimamizi wa mirathi wenye ujuzi na uzoefu wa muda mrefu, Uzoefu unaonyesha kwamba inakuwa vigumu kutekeleza majukumu ya usimamizi wa mirathi pasipo kuwa na wosia.

4. RITA inatoa huduma nzuri, kwa urahisi na gharama nafuu,ambayo kila mwananchi ataweza kuimudu.

5. RITA ina Ofisi katika wilaya zote Tanzania bara hivyo itakuwa rahisi kuwafikia wananchi wengi na kufaidika na huduma hii.

Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia Wajane na Watoto wa marehemu wakipoteza haki zao kwa waume kufa bila kuacha Wosia.Hata wale ambao wametayarisha wosia wanakuwa hawahifadhi mahali salama matokeo yake ni kupoteza haki na malengo husika.
Pia wananchi wengi hawafahamu sehemu za kutunza Wosia kama Mahakama Kuu au Benki. Hata wachache wanaozifahamu wanashindwa kufanya hivyo kutokana na gharama za kutunzia wosia kuwa kubwa.
RITA kama msimamizi wa haki za urithi na nyinginezo inao wajibu kuona kwamba haki za Urithi zinalindwa kwa misingi hiyo imeanzisha kitengo cha Wosia ambacho kitashughulika na kuandika na kutunza Wosia kwa huduma nzuri,usiri na gharama nafuu ambayo kila mwananchi ataweza kumudu.

## WOSIA
## MAANA YA WOSIA

Ni tamko au maandishi anayotoa mtu wakati wa uhai wake akielezea mazishi yake yatakavyofanyika likionyesha mahali atakapozikwa au jinsi mali zake zitakavyogawiwa kwa warithi wake baada ya kifo chake.

### AINA ZA WOSIA

Kuna aina mbili za Wosia;

1. Wosia wa maandishi
2. Wosia wa mdomo/matamshi

### TARATIBU ZA KUANDIKA WOSIA

Taratibu za kuandika wosia zinatofautiana kulingana na sheria ya mirathi inayotumika.

### 1. WOSIA WA MAANDISHI

- Wosia huu unashuhudiwa na watu wawili pale ambapo mtoa wosia anajua kusoma au kuandika. Shuhuda mmoja lazima awe ndugu wa karibu wa mtoa wosia na mwingine ambaye sio ndugu wa karibu.Wosia na unatakiwa uwe na tarehe, uandikwe kwa karamu ya wino au upigwe chapa na uwe na saini ya mtoa wosia na saini za mashuhuda ambapo wote wanatakiwa kutia saini zao kwa wakati mmoja.
- Mtoa wosia asiye jua kusoma ua kuandika awe na mashuhuda wa nne wanao jua kusoma na kuandika,muhusia huyo aweke alama ya kidole gumba cha mkono wake wa kulia,mashuhuda hao wote washuhudie na waweke saini zao kwenye Wosia kwa wakati mmoja.

## 2. WOSIA WA MDOMO/MATAMSHI

- Wosia huu unashuhudiwa na mashuhuda wasiopungua wa nne wawili kati yao ndugu wa mtoa wosia na wawili waliobaki wasio ndugu wa mtoa wosia.Wosia huu utolewa na mtu asiye jua kusoma na kuandika.

## TARATIBU ZA KUANDIKA WOSIA KATIKA SHERIA ZA MIRATHI

- Wosia katika Sheria za kimila,zipo katika jedwali la 3 la Sheria ya (The Local Customary Law (Declaration|) No. 4 Order,1963.

- Wosia katika Sheria za kiserikali,zipo katika sheria iliyorithiwa kutoka kwa Waingereza ya(The Indian Succession Act ),iliyopitishwa huko India mwaka 1865

    - Hauna tofauti kubwa na wosia wa kimila isipokuwa wosia huu unatakiwa uwe katika maandishi.Vipengele vyote vya wosia wa maandishi vinatumika.
    - Mtoa wosia anaweza kufuta au kuongeza maneno mengine kwa kuandika maandishi mengine ambayo yatatakiwa kuzingatia masharti ya uandikaji wosia.

- Wosia katika Sheria za kiislamu, mtoa wosia anaruhusiwa kuuusia 1/3 ya mali yake 2/3 lazima irithiwe na warithi halali.

## UMUHIMU WA KUANDIKA WOSIA

- Unaweka mambo bayana kuondoa utata kwa familia na jamaa zako.
- Unamchagua msimamizi wa mirathi unayemtaka wewe.
- Unatoa maelezo ya wapi mwili wako uhifadhiwe, taratibu zitakazotumika kuuzika mwili wako na jinsi gani mali yako igawanywe kama upendavyo wewe na kwa mujibu wa Sheria.

## MASHARTI YA WOSIA

- Mtoa wosia lazima awe na akili timamu.
- Awe ametimiza miaka kumi na nane (18) na kuendelea.
- Uonyeshe tarehe,mwezi na mwaka ulioandikwa.
- Uonyeshe majina ya warithi.
- Mtoa wosia ahusishe mali zake binafsi na si za mtu mwingine.
- Wosia ni siri wanufaika hawatakiwi kuujua.
- Ushuhudiwe na mashaidi wawili, kwa mtoa wosia anaye jua kusoma na kuandika na kwa yule asiye jua kusoma ua kuandika mashuhuda wake lazima wawe wanne na wajue kusoma na kuandika.
- Mtoa wosia lazima aweke saini yake,na kama hajui kusoma na kuandiaka aweke alama ya dole gumba la mkono wa kulia.
- Mashuhuda lazima waweke saini zao tena kwa wakati mmoja.

**SABABU ZINAZOWEZA KUSABABISHA MTOA WOSIA KUTOMRITHISHA MRITHI WAKE**

1. Kumtelekeza mtoa wosia pale ambapo anaumwa na kuhitaji msaada.
2. Kufanya uzinzi na mke wa mtoa wosia.
3. Endapo kifo cha mtoa wosia kitakuwa kimesababishwa na mrithi.

**GHARAMA ZA KUANDIKA NA KUTUNZA WOSIA RITA**

Gharama zetu za kuandika na kutunza wosia zimezingatia makundi kama yafuatavyo;-

1. **THAMANI YA MALI: 0 -50,000,000**
   Kutayarisha : 5,000/=
   Kutunza : 5,000/=
   Marekebisho: 5,000/=

2. **THAMANI YA MALI: 51,000,000-200,000,000**
   Kutayarisha: 20,000/=
   Kutunza : 20,000/=
   Marekebisho: 20,000/=

3. **THAMANI YA MALI: 201,000,000- 500,000,000**
   Kutayarisha : 30,000/=
   Kutunza : 30,000/=
   Marekebisho: 30,000/=

4. **THAMANI YA MALI: 501,000,000- Nakuendelea**
   Kutayarisha : 50,000/=
   Kutunza : 50,000/=
   Marekebisho: 50,000/=

Wasiliana na RITA kupitia anuani zifuatazo:

Afisa Mtendaji Mkuu/Kabidhi Wasii Mkuu
Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini(RITA)
Mtaa wa Kipalapala,Kiwanja Na.516
Upanga
S.L.P 9183
Dar es Salaam.
Simu Namba +255 - 22 – 2153069
Nukushi+255-22-2153075

Au waweza kutembelea tovuti yetu
www.rita.go.tz